**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# TAARIFA YA MAENDELEO YA UJENZI WA MFUMO WA TAKWIMU ZA KITAIFA KATIKA SEKTA YA ELIMU

**JANUARI 2026**

# YALIYOMO


Orodha ya Vifupisho na Maana Zake ..... ii

Muhtasari wa Taarifa ..... iii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ..... 1

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Malengo ya Mfumo ..... 2

1.2.1 Malengo Mahususi ..... 2

1.3 Mawanda ya Mfumo ..... 3

1.4 Mifumo iliyounganishwa na ESMIS ..... 3

1.5 Muundo wa Mfumo ..... 3

SURA YA PILI: MAENDELEO YA UJENZI WA MFUMO ..... 6

2.1 Maendeleo ya Ujenzi wa Mfumo ..... 6

2.2 Ujumuishaji na Usimamizi wa Takwimu (Data Integration and Management) ..... 7

2.3 Miundombinu na Uwekaji wa Mfumo Hewani (Infrastructure and Deployment) ..... 8

SURA YA TATU: MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA HATUA ZINAZOFUATA ..... 9

3.1 Mafanikio ..... 9

3.2 Changamoto na Utatuzi ..... 11

3.3 Hatua Zinazoendelea Kutekelezwa ..... 12

3.4 Hitimisho ..... 13

Kiambatisho 1: Hali ya Uunganishaji wa Mifumo ..... 14

# Orodha ya Vifupisho na Maana Zake

| **Kifupisho** | **Maana Kamili** |
|---|---|
| AI | Artificial Intelligence |
| BEST | Basic Education Statistics |
| CIA | Confidentiality, Integrity, and Availability |
| COSTECH | Commission for Science and Technology |
| e-GA | e-Government Authority |
| ESMIS | Education Sector Management Information System |
| HESLB | Higher Education Students Loans Board |
| HESLIS | Higher Education Students' Loans Information System |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| NACTVET | National Council for Technical and Vocational Education and Training |
| NECTA | National Examinations Council of Tanzania |
| NIDC | National Internet Data Centre |
| NISSTI | National Information System for Science, Technology, and Innovation |
| OSMIS | Open Schools Management Information System |
| OWM–TAMISEMI | Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| SAS | School Accreditation System |
| SDD | System Design Document |
| SIS | School Information System |
| SRS | System Requirements Specifications |
| STI | Science, Technology, and Innovation |
| TCU | Tanzania Commission for Universities |
| TEMIS | Tertiary Education Management Information System |
| UAT | User Acceptance Test |
| UIMS | University Information Management System |
| VAPT | Vulnerability Assessment and Penetration Testing |

# Muhtasari wa Taarifa

Taarifa hii inawasilisha maendeleo ya ujenzi wa Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu za Sekta ya Elimu (ESMIS) kwa kipindi kinachoishia Desemba, 2025. Lengo kuu la ujenzi wa mfumo huu ni kuwa na chanzo kimoja cha takwimu na viashiria muhimu vya sekta ya elimu ili kuwezesha upangaji, utungaji wa sera, na ugawaji wa rasilimali kwa ushahidi na kuzingatia uhalisia.

Sekta ya elimu imekuwa ikitumia mifumo mingi isiyounganishwa, hali iliyosababisha takwimu zisizo linganifu, zisizo kamilifu na kuchelewa kupatikana. Hali hii imekuwa kikwazo katika kupanga mipango, kutathmini sera na kufanya maamuzi sahihi ya kimkakati.

ESMIS ni mfumo mmoja wa kitaifa unaounganisha mifumo 12 ya takwimu za elimu (shule, vyuo, walimu, wanafunzi, mikopo, mitihani n.k.) na kuwa chanzo kimoja cha kuaminika cha takwimu za elimu nchini. Mfumo ni utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 (Toleo la 2023). Kupitia mfumo wa ESMIS, watumiaji wa mfumo wataweza:

- Kufanya maamuzi ya haraka na sahihi yanayotegemea ushahidi wa takwimu;
- Kuimarisha mipango, sera na matumizi ya rasilimali katika sekta ya elimu;
- Kufuatilia utendaji wa sekta ya elimu kulingana na wakati husika, na
- Kuongeza uwazi na uwajibikaji wa taasisi zilizopo katika sekya ya elimu.

Hadi kufikia Disemba 2025, hali ya utengenezaji wa mfumo wa ESMIS ni kama ifwatavyo:

- Moduli 8 kati ya 9 zimekamilika na zinafanya kazi vizuri.
- Takwimu zote kutoka vitabu vya BEST kuanzia mwaka 2020 – 2024 zimesafishwa, zimehamishwa na sasa zinapatikana katika mfumo wa ESMIS.
- Mfumo umeunganishwa na mifumo yote muhimu katika sekta ya elimu.

- Mfumo umehifadhiwa salama katika miundombinu ya NIDC kulingana na miongozo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao.
- Moduli ya Tafiti na Bunifu katika mfumo wa ESMIS inasubiri kukamilika kwa Mfumo wa Kitaifa wa Tafiti na Bunifu wa COSTECH.

Kulingana na malengo mahususi ya kazi hii, yafuatayo ni mafanikio ya muhimu na msingi yaliyoweza kufikiwa mpaka sasa:
Kuwepo kwa mfumo mmoja (ESMIS) kupitia esmis.moe.go.tz/ utakao kusanya, kuchakata na kuhifadhi takwimu zote muhimu za sekta ya elimu (shule, wanafunzi, walimu, miundombinu, n.k.).

- Kukamilika kwa Rasimu ya Mwongozo wa Usimamizi wa Takwimu katika Sekta ya Elimu unaotoa maelekezo kwa taasisi zote zinazozalisha takwimu katika sekta ya elimu kuhusu utaratibu wa ukusanyaji wa takwimu zinazohitajika katika mfumo wa ESMIS.

Changamoto zilizobaki na mpango wa sasa tunaopendekeza kwa ajili ya kuzitatua changamoto hizi ni kama ifuatavyo:

- Baadhi ya takwimu bado hazikusanywi katika baadhi ya mifumo ya sekta ya elimu hali inayopelekea takwimu za sasa katika mfumo wa ESMIS kutokuwa kamilifu kulingana na mahitaji ya sekta ya elimu. Hata hivyo, Rasimu ya Mwongozo wa Usimamizi wa Takwimu katika Sekta ya Elimu umeandaliwa na utekelezaji wake utasaidia upatikanaji wa takwimu katika sekta ya elimu kwa usahihi, ukamilifu na wakati kusudiwa.
- Mfumo wa Tafiti na Bunifu (COSTECH) bado haujakamilika. Hata hivyo, mfumo wa ESMIS unaweza kuanza kutumika kwa moduli zilizo tayari. Mfumo wa Tafiri na Bunifu utaunganishwa na ESMIS mara tu utakapokamilika.

Mfumo umewasilishwa kwa Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Mwenyekiti wa Kamati Maalumu, na mapendekezo ya maboresho yamepokelewa. Baadhi yametekelezwa na mengine yanaendelea kufanyiwa kazi, yakitarajiwa kukamilika ifikapo 31 Januari 2026.

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

Sehemu hii inaelezea Utangulizi, malengo na mawanda (Scope) ya Mfumo wa ESMIS.

**1.1 Utangulizi**

Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu za Sekta ya Elimu (Education Sector Managment Information System - ESMIS) ni mfumo wa kimkakati wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ulioundwa ili kuunganisha mifumo yote ya elimu na kuwa chanzo kimoja cha uhakika cha taarifa na takwimu za sekta ya elimu nchini. Mfumo huu unalenga kusaidia maamuzi ya kisera, upangaji wa mipango, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya elimu.

Ujenzi wa ESMIS ulianza kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda (MB), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, aliyeteua Kamati Maalum ya Kitaifa tarehe 9 Agosti 2024. Kamati hiyo, iliyoongozwa na Prof. Said Ally Mohamed, Katibu Mtendaji wa NECTA, ilipewa jukumu la kusimamia ujenzi wa mfumo jumuishi wa takwimu za elimu na kuhakikisha unakidhi mahitaji ya Serikali kwa ujumla.

Kabla ya kuanzishwa kwa ESMIS, Serikali ilikuwa ikitumia mifumo mbalimbali ya elimu ambayo haikuwa imeunganishwa. Hali hii ilisababisha changamoto za utofauti wa takwimu, ucheleweshaji wa taarifa, na wakati mwingine kutokuwepo kwa takwimu sahihi kwa ajili ya maamuzi ya haraka. Kutokana na changamoto hizo, kumekuwa na umuhimu wa kuwa na mfumo madhubuti wa kukusanya, kuhakiki, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza takwimu na taarifa zote muhimu zinazohusu sekta ya elimu kwani hatua zote za mipango ya elimu zinategemea uwepo wa taarifa na takwimu sahihi na zenye ubora, zilizochanganuliwa kwa kuzingatia vigezo vyote muhimu.

Aidha, ujenzi wa ESMIS unatekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, hususan tamko la 3.15.1 linalosisitiza uwepo wa mfumo unganifu wa taarifa na takwimu za elimu katika ngazi zote. Hivyo, ESMIS ni chombo muhimu cha utekelezaji wa sera na mageuzi ya usimamizi wa sekta ya elimu.

### 1.2 Malengo ya Mfumo

Lengo kuu la ESMIS ni kuwezesha upatikanaji wa takwimu sahihi, kamilifu na haraka kwa ajili ya maamuzi ya menejimenti, upangaji wa mipango na ufuatiliaji wa maendeleo ya sekta ya elimu.

#### 1.2.1 Malengo Mahususi

(i) **Kukusanya, kuchakata na kuhifadhi takwimu zote za elimu katika mfumo mmoja wa kitaifa**: ESMIS inalenga kuwa chanzo kimoja cha taarifa zote za elimu nchini. Kupitia mfumo huu, takwimu zote muhimu zinazohusu shule, wanafunzi, walimu, miundombinu na rasilimali nyingine hukusanywa, huchakatwa na kuhifadhiwa mahali pamoja ili kuondoa mgawanyiko wa taarifa uliokuwepo awali.

(ii) **Kuimarisha ubora wa takwimu za elimu**: ESMIS itaimarisha taratibu za ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na utumiaji wa takwimu kwa kutoa mwongozo wa ukusanyaji, mahitaji ya takwimu pamoja na muda wa ukusanyaji takwimu kwa lengo la kuimarisha ubora wa takwimu.

(iii) **Kuwezesha upatikanaji wa taarifa na ripoti kwa wakati**: Kupitia ESMIS, menejimenti ya Wizara na wadau wengine watapata takwimu za elimu na ripoti kwa haraka bila kusubiri michakato mirefu ya ukusanyaji wa takwimu kutoka vyanzo tofauti. Hii itaongeza ufanisi katika kufanya maamuzi ya haraka na ya msingi.

(iv) **Kusaidia upangaji wa sera, mipango ya maendeleo na matumizi bora ya rasilimali**: Upatikanaji wa takwimu za elimu za sahihi na kwa wakati utaiwezesha Wizara kupanga mipango ya maendeleo kwa kuzingatia ushahidi wa takwimu, kufuatilia utekelezaji wa sera, pamoja na kuhakikisha rasilimali za Serikali zinatumika kwa tija kulingana na mahitaji halisi ya sekta ya elimu.

### 1.3 Mawanda ya Mfumo

ESMIS inahusisha takwimu za elimu kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya juu, pamoja na elimu nje ya mfumo rasmi, elimu ya ualimu, mikopo ya wanafunzi, na taarifa za tafiti na bunifu. Mfumo umeundwa ili kuunganisha mifumo ya taasisi mbalimbali zinazozalisha takwimu za elimu nchini.

Aidha, mfumo unalenga kutumika kwa wadau wote wenye lengo la kujua hali ya elimu nchini ambapo vitabu vya takwimu za elimu (BEST) vitapatikana kwa urahisi pale inapohitajika. Vilevile, mfumo huu utaweza kuhudumia viongozi na maafisa watakaopatiwa nywila ili waweze kupata takwimu zote za elimu. Hata hivyo, kwa kuzingatia malengo ya mfumo huu takwimu kutoka katika ngazi zote za elimu ikiwemo elimu ya awali, shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya kati, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, vyuo vya elimu ya juu, takwimu za mikopo kwa wanafunzi, na takwimu za tafiti na bunifu mbalimbali zitapatikana katika mfumo huu.

### 1.4 Mifumo iliyounganishwa na ESMIS

Mfumo huu wa ESMIS unapatikana kupitia tovuti ya esmis.moe.go.tz/ ambao umejengwa kwa kuunganisha mifumo mingine 12 ya takwimu za elimu kutoka taasisi mbalimbali katika sekta ya elimu. Mifumo hiyo inahusisha elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, vyuo vya kati, vyuo vikuu, elimu ya ufundi, elimu ya ualimu, elimu nje ya mfumo rasmi, pamoja na mfumo wa mikopo ya wanafunzi. Uunganishaji huu umewezesha kupatikana kwa takwimu kwa mtiririko mmoja na kwa viwango vinavyofanana. Orodha kamili ya mifumo imeainishwa katika **Kiambata Na. 1**.

### 1.5 Muundo wa Mfumo

ESMIS umeundwa katika sehemu kuu mbili zinazokidhi mahitaji ya makundi tofauti ya watumiaji:

(a) Sehemu ya takwimu kwa ajili ya Umma

Sehemu hii inawezesha mwananchi na mtu mwingine yeyote kuweza kuona na kutumia takwimu mbalimbali za elimu zilizoruhusiwa kutumika kwa matumizi ya umma. Takwimu hizi zinajumuisha upatikanaji wa vitabu vya BEST kwa umma bila kuhitaji nywila. Lengo ni kuongeza uwazi na matumizi ya takwimu katika jamii.

(b) Sehemu ya takwimu kwa ajili ya matumizi ya ndani

Sehemu hii inawezesha viongozi na maafisa wa sekta ya elimu ambao wamepatiwa nywila kuweza kupata takwimu zote za elimu kwa upana. Sehemu hii imepangiliwa katika moduli kuu tisa (9) ambazo ni:

(i) **Moduli ya Dashibodi** inayolenga kutoa muhtasari (Overview) ya takwimu zote za sekta ya elimu ambapo takwimu muhimu ikiwemo udahili wa wanafunzi na idadi ya walimu katika ngazi zote zinapatikana. Aidha, takwimu hizi zitarahisisha upatikanaji wa takwimu za elimu kwa mtumiaji wa mfumo kwa haraka zaidi kabla ya kwenda kwenye moduli husika.

(ii) **Moduli ya Elimu Msingi** inayolenga kutoa takwimu zote za elimu ya awali, elimu ya msingi, sekondari ya chini na sekondari ya juu. Aidha, takwimu hizi zimegawanywa katika moduli ndogo ndogo (sub-module) ambazo ni Viashiria (Indicators), Shule (Schools), Mbinu na Nadharia za Ufundishaji (Pedagogy), Walimu (Teachers), Miundombinu (Infrastructures), Wanafunzi (Students), na Upimaji (Assessment).

(iii) **Moduli ya Elimu ya Ualimu** inayohusisha takwimu za walimu ambapo takwimu zimegawanywa katika moduli ndogo ndogo (sub moduli) ambazo ni taasisi (institutions), Watumishi (Staff) na Wanafunzi (Students).

(iv) **Moduli ya Elimu ya Nje ya Mfumo Rasmi** inayohusisha takwimu za elimu nje ya mfumo rasmi kutoka taasisi ya elimu ya watu

wazima ambapo takwimu zimegawanywa katika moduli ndogondogo ambazo ni viashiria (Indicators), taasisi (institutions), watumishi (staff) na wanafunzi (students).

(v) **Moduli ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu** inayohusisha takwimu za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka bodi ya mikopo. Aidha, takwimu hizo zimegawanywa katika moduli ndogondogo nne yaani loans application, loans beneficiaries, loans repayment na loans disbursement.

(vi) **Moduli ya Elimu ya Juu na Vyuo vya Kati** (Tertiary Education) inayohusisha takwimu za elimu baada ya sekondari ambapo takwimu za vyuo vya kati na vyuo vikuu vimejumuishwa. Aidha, takwimu katika moduli hii zimegawanywa katika moduli ndogondogo ambazo ni viashiria, taasisi, watumishi na wanafunzi.

(vii) **Moduli ya Ripoti** iliyoundwa mahususi kwa ajili ya kutoa ripoti za takwimu mbalimbali zinazopatikana ndani ya mfumo huu ni kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa takwimu.

(viii) **Moduli Usimamizi wa Mfumo (System Administration)** kwa ajili ya kufanya mipangilio (settings) mbalimbali za Mfumo ambapo mmiliki wa mfumo (System Administrator) ataweza kufanya marekebisho mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuruhusu takwimu gani ziweze kuoneka kwa umma.

(ix) **Moduli ya Tafiti na Bunifu** inalenga kutoa takwimu za tafiti na bunifu mbalimbali zinazofanyika kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia.

# SURA YA PILI: MAENDELEO YA UJENZI WA MFUMO

Sehemu hii inatoa taarifa ya kina kuhusu maendeleo yaliyofikiwa katika maeneo makuu ya ujenzi wa mfumo.

### 2.1 Maendeleo ya Ujenzi wa Mfumo

Hadi kufikia Desemba 2025, moduli nane (8) kati ya tisa (9) zimekamilika na zipo tayari kuwa matumizi. Moduli ya Tafiti na Bunifu haijakamilika kutokana na kuchelewa kukamilika kwa mfumo wa COSTECH kama inavyoainishwa katika Jedwali Namba 1.

***Jedwali 1:*** *Muhtasari wa ujumla wa maendeleo ya Ujenzi wa Mfumo wa ESMIS*

| Na | Moduli Kuu | Hali | % Iliyokamilika | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Dashibodi | Imekamilika | 100% | |
| 2 | Usimamizi wa Watumiaji | Imekamilika | 100% | |
| 3 | Elimu Msingi | Imekamilika | 100% | |
| 4 | Elimu ya Ualimu | Imekamilika | 100% | |
| 5 | Elimu ya Juu na Vyuo vya Kati (Tertiary Education) | Imekamilika | 100% | |
| 6 | Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) | Imekamilika | 100% | |

| Na | Moduli Kuu | Hali | % Iliyokamilika | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 7 | Utafiti na Ubunifu | Haijaanza | 0% | Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu za Utafiti na Bunifu bado unaandaliwa na COSTECH. |
| 8 | Usimamizi wa Mfumo (System Administration) | Imekamilika | 100% | |
| 9 | Ripoti | Imekamilika | 100% | |

Aidha, mfumo huu wa ESMIS umeshawasilishwa kwa menejimenti ya Wizara pamoja na Mwenyekiti wa Kamati Maalum kwa ajili ya mapitio. Kufuatia mawasilisho hayo mawili, maoni, mapendekezo na maboresho mbalimbali yamepokelewa, kuchambuliwa na kuanza kufanyiwa kazi.

**2.2 Ujumuishaji na Usimamizi wa Takwimu (Data Integration and Management)**

Katika eneo la ujumuishaji na usimamizi wa takwimu, shughuli kuu zifuatazo zimefanyika:

(i) **Uhamishaji wa Takwimu (Data Migration):**

Zoezi la uhamishaji wa takwimu za miaka mitano (2020 hadi 2024) limekamilika. Aidha,Takwimu za viashiria vyote muhimu, ikiwemo uandikishaji wa wanafunzi na takwimu za walimu zinapatikana katika mfumo na tayari kwa matumizi.

(ii) **Tathmini na Usafishaji wa Takwimu (Data Quality Assessment & Cleaning)**:

Tathmini ya kina ya takwimu zote zilizoingizwa kwenye mfumo imefanyika na kukamilika, na hatua za usafishaji takwimu zimechukuliwa. Aidha, kumebainika kuwepo kwa mapungufu katika baadhi ya viashiria na takwimu za sekta ya elimu yanayotokana na changamoto katika mifumo na taratibu zilizokuwa zikitumika kukusanya na kuchakata (manual data collection and analysis) takwimu za elimu. Pia, katika zoezi hili, ilibainika baadhi ya takwimu hazikupatikana kwani bado hazikusanywi katika mifumo ya sekta ya elimu iliyopo sasa. Ilishauriwa kuelekeza taasisi zinazosimamia mifumo husika kuanza kukusanya takwimu zinazohitajika.

Hata hivyo, ili kuondokana na changamoto hizi, Wizara imeandaa na kukamilisha Rasimu ya Mwongozo wa Usimamizi wa Takwimu katika Sekta ya Elimu ambazo zitakuwa zikipatikana katika mfumo kwa lengo la kuhakikisha usahihi, ukamilifu na ulinganifu wa takwimu katika sekta ya elimu.

(iii) **Uunganishaji wa Mifumo ya Nje**:
Kazi ya kuunganisha ESMIS na mifumo muhimu ya nje imekamilika na ipo katika matumizi rasmi. Aidha, ujumuishaji na mifumo ya UIMS (TCU), NACTVET, TCMS, SAS, SQAS, NECTA na SIS pamoja na mifumo mingine husika umekamilika kikamilifu na inafanya kazi kwa ufanisi. Hivyo, inawezesha upatikanaji wa takwimu kulingana na Rasimu ya Mwongozo wa Usimamizi wa Takwimu katika Sekta ya Elimu.

**2.3 Miundombinu na Uwekaji wa Mfumo Hewani (Infrastructure and Deployment)**

Katika kuhakikisha mfumo wa ESMIS ni salama na miundombinu ya mifumo ni imara mambo yafuatayo yamefanyika:

(i) Mfumo wa ESMIS unahifadhiwa kwenye Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data (National Internet Data Centre - NIDC) kama ilivyo kwa mifumo mingine ya Serikali. Hii inahakikisha usalama na upatikanaji wake muda wote.

(ii) Kuhifadhiwa katika kituo cha NIDC pia kunaimarisha usalama wa ESMIS, ikiwemo udhibiti wa ufikiaji wa mfumo kwa kutumia majukumu (role-based access controls), usimbaji wa data (data encryption) wakati wa usafirishaji na uhifadhi, pamoja na kufuata miongozo yote ya usalama wa mitandao iliyotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Hatua hizi zitasaidia kulinda takwimu mbalimbali zinazohifadhiwa katika mfumo wa ESMIS.

# SURA YA TATU: MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA HATUA ZINAZOFUATA

Sehemu hii inatoa taarifa ya mafanikio yaliyopatikana mpaka sasa, changamoto zilizojitokeza na utatuzi wa changamoto hizo, hatua zinayofuata katika kuhakikisha mfumo unaanza kutumika pamoja na hitimisho

### 3.1 Mafanikio

Hadi kufikia Desemba, 2025 kamati maalum pamoja na timu ya wataalamu imefanikiwa mambo yafuatayo:

(i) **Kukamilika kwa nyaraka muhimu za mfumo (SRS na SDD):** Nyaraka za System Requirements Specifications (SRS) na System Design Document (SDD) zimekamilika na kuidhinishwa. Nyaraka hizi zimeainisha kwa uwazi mahitaji ya mfumo, usanifu wake, mtiririko wa taarifa na majukumu ya moduli mbalimbali. Hii imewezesha timu ya ufundi kujenga mfumo kwa mwelekeo unaokidhi mahitaji ya Wizara na viwango vinavyokubalika;


(ii) **Kukamilika kwa Rasimu ya Mwongozo wa Uzalishaji wa Takwimu za Sekta ya Elimu:** Timu ya wataalamu imekamilisha kuandaa Rasimu ya Mwongozo wa Uzalishaji wa Takwimu za Sekta ya Elimu kwa lengo la kuweka utaratibu wa pamoja wa ukusanyaji, uchakataji na utoaji wa takwimu. Mwongozo huu umebainisha aina za takwimu zinazopaswa kukusanywa, taasisi husika na muda wa ukusanyaji. Rasimu hiyo iliwasilishwa kwa Katibu

Mkuu ambaye alitoa maoni na maboresho yanayoendelea kufanyiwa kazi na timu ya wataalamu;

(iii) **Kuwasilisha kwa Mfumo wa ESMIS kwa Menejimenti ya Wizara na kupokea maoni:** Mfumo wa ESMIS uliwasilishwa kwa Katibu Mkuu (KM) na Menejimenti ya Wizara kwa nyakati tofauti. Kupitia mawasilisho hayo, maoni na mapendekezo mbalimbali yalitolewa ikiwemo kuimarisha upatikanaji wa takwimu muhimu, kuboresha muonekano wa mfumo, pamoja na pendekezo la kuunganisha mfumo na teknolojia za Akili Unde (AI). Maoni hayo yamechambuliwa na utekelezaji wake unaendelea.

(iv) **Kuwasilishwa kwa Mfumo wa ESMIS kwa Mwenyekiti wa Kamati Maalum:** Mfumo wa ESMIS uliwasilishwa kwa Mwenyekiti wa Kamati Maalum, Prof. Saidi A. Mohamed, tarehe 19.12.2025, Dodoma. Mwenyekiti alitoa maelekezo na mapendekezo ya kimkakati yaliyojikita katika matumizi ya mfumo kwa maamuzi ya sera na ufuatiliaji wa sekta ya elimu. Timu ya wataalamu inaendelea kuyafanyia kazi maelekezo na maoni hayo.

(v) **Kukamilika kwa Ujenzi wa Mfumo ESMIS:** Ujenzi wa mfumo wa ESMIS umekamilika katika moduli kuu nane (8) ambazo ni Dashibodi, Usimamizi wa Watumiaji, Elimu Msingi, Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, Elimu ya Ualimu, Elimu ya Juu na Vyuo vya Kati (Tertiary Education), Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) pamoja na Moduli ya Ripoti. Moduli hizi zipo katika hali ya kufanya kazi vizuri na zinatoa takwimu zinazoweza kutumika kwa uchambuzi, usimamizi na maamuzi ya kiutawala na kisera kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 1.




Kielelezo 1: Muonekano wa Mfumo wa ESMIS

### 3.2 Changamoto na Utatuzi

Katika utekelezaji wa ujenzi wa mfumo, changamoto zifuatazo zimebainika, na hatua za kukabiliana nazo zinapendekezwa kama inavyosomeka kwenye Jendwali Na. 2.

***Jedwali 2****:* Muhtasari wa changamoto na mapendekezo kwa ajili ya maboresho

| Na | Changamoto | Utatuzi |
|---|---|---|
| 1. | Kukosekana kwa baadhi ya takwimu katika baadhi ya mifumo ya sekta ya elimu hali inayopelekea takwimu za sasa katika mfumo wa ESMIS kutokuwa kamilifu kulingana na mahitaji ya sekta ya elimu. | Wizara imeandaa Rasimu ya Mwongozo wa Usimamizi wa Takwimu katika Sekta ya Elimu unaotoa maelekezo kwa taasisi zote zinazozalisha takwimu katika sekta ya elimu kuhusu utaratibu wa ukusanyaji wa takwimu zinazohitajika katika mfumo wa ESMIS. |

| Na | Changamoto | Utatuzi |
|---|---|---|
| 2. | Kutokamilika kwa Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu za Tafiti na Bunifu kutoka COSTECH ambao unatarajiwa kuunganishwa na ESMIS. | COSTECH wameandikiwa barua ya kuhimizwa kukamilisha mfumo huo ili kuhakikisha mfumo wa ESMIS unakuwa na takwimu zote muhimu katika sekta ya elimu. |

**3.3 Hatua Zinazoendelea Kutekelezwa**

Katika kuhakikisha ESMIS inaanza kutumika kikamilifu na kwa ufanisi endelevu, Kamati Maalum na Timu ya Wataalamu zinaendelea kutekeleza hatua zifuatazo:

(i) **Kutekeleza maboresho yaliyopendekezwa**: Maboresho yote yaliyopokelewa kutoka kwa Katibu Mkuu, Menejimenti ya Wizara na Mwenyekiti wa Kamati Maalumu yanaendelea kufanyiwa kazi. Maboresho haya yanalenga kuhakikisha mfumo unakidhi mahitaji ya watumiaji wa ngazi zote.

(ii) **Kuimarisha ubora wa takwimu:** Timu ya wataalamu inaendelea kushirikiana na taasisi zinazosimamia mifumo ya takwmu katika sekta ya elimu ili kuimarisha taratibu za uhakiki, usafishaji na ufuatiliaji wa ubora wa takwimu. Lengo ni kuhakikisha takwimu zinazopatikana kupitia ESMIS ni sahihi, kamili na za kuaminika kwa matumizi ya kitaalamu na kiutawala.

(iii) **Upimaji wa Mfumo kwa Watumiaji (User Acceptance Test - UAT):** Upimaji wa mfumo kwa kushirikisha watumiaji halisi utafanyika ili kuthibitisha kuwa mfumo unafanya kazi kama ilivyokusudiwa na unakidhi matarajio ya watumiaji kabla ya kuanza matumizi rasmi kwa walengwa.

(iv) **Tathmini ya Usalama wa Mfumo:** Tathmini ya kina ya usalama wa ESMIS itafanyika kwa kuzingatia miongozo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA). Tathmini hii itajumuisha ukaguzi wa miundombinu, udhibiti wa upatikanaji wa taarifa, usalama wa data, pamoja na utekelezaji wa Vulnerability Assessment and Penetration Testing (VAPT). Matokeo ya tathmini yatatumika kuboresha usalama wa mfumo na kuhakikisha matumizi yake ni salama na endelevu.

### 3.4 Hitimisho

Kwa ujumla, ujenzi wa Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu za Sekta ya Elimu (ESMIS) umefikia hatua ya kuridhisha, ambapo mifumo muhimu ya sekta ya elimu imeunganishwa na kuwezesha upatikanaji wa takwimu kwa usahihi, ukamilifu na wakati kusudiwa, kwa njia jumuishi na salama. Hatua hii ni utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, inayosisitiza uwepo wa mfumo mmoja wa kitaifa wa taarifa na takwimu za elimu kwa ajili ya upangaji, ufuatiliaji, tathmini ya sera na matumizi bora ya rasilimali kwa kuzingatia ushahidi.

Hata hivyo, ili kuhakikisha ESMIS inatumika kikamilifu na kwa ufanisi endelevu, kuna umuhimu wa kuendelea kukamilisha maboresho yanayoendelea, hususan ujumuishaji wa mifumo ambayo bado haijakamilika, uimarishaji wa taratibu za uthibitishaji na usimamizi wa ubora wa takwimu, pamoja na kuwajengea uwezo watumiaji wa mfumo katika ngazi zote. Kwa kuhitimisha, ESMIS inatarajiwa kuwa chombo cha kimkakati katika kuimarisha uwazi, uwajibikaji na matumizi ya takwimu katika maamuzi ya kisera na kiutawala, hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta ya elimu na taifa kwa ujumla.

**Kiambatisho 1: Hali ya Uunganishaji wa Mifumo**

| Na. | Mfumo Chanzo (Producer) | Mfumo Lengwa (Consumer) | Hali | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | UIMS (TEMIS) | ESMIS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za TCU kwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) |
| 2 | TCMS | SQAS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za Vyuo vya Ualimu kwenda kwenye Mfumo wa Uhakiki wa Ubora (SQA) |
| 3 | SAS | SIS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za usajili wa shule kwenda Ofisi ya Rais – TAMISEMI |
| 4 | SAS | SQAS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za usajili wa shule kwenda kwenye Mfumo wa Uhakiki wa Ubora (SQA) |
| 5 | SAS | PREM | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za usajili wa shule kwenda NECTA kwa ajili ya upimaji wa shule za msingi |
| 6 | SAS | TCMS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za usajili wa Vyuo vya Ualimu kwenda kwenye Mfumo wa Vyuo vya Ualimu |
| 7 | SAS | PREMS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za usajili wa shule kwenda NECTA kwa ajili ya upimaji wa shule za sekondari |
| 8 | API ya Matokeo ya NECTA | TCMS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa matokeo ya wanafunzi wa Vyuo vya Ualimu kwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| 9 | NACTVET (TEMIS) | ESMIS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za NACTVET kwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| 10 | HESLB (TEMIS) | ESMIS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi kwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| 11 | OSMIS | ESMIS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za elimu nje ya mfumo rasmi |
| 12 | SIS | SQAS | Uunganishaji umekamilika | Ugawaji wa takwimu za shule, walimu na wanafunzi kwenda kwenye Mfumo wa Uhakiki wa Ubora (SQA) |